



St. Walburg's Hospital Nyangao

P. O. Box. 1002, Lindi Region - Tanzania, Mobile no. +255656227511
Email address: nyangaohospital@gmail.com Website: <http://www.nyangaohospital.or.tz>

10/11/2025

TANGAZO LA KAZI

Hospitali ya Rufaa ya Mt.Walburga Nyangao iliyoko Jimbo Katoliki la Lindi inatangaza nafasi za kazi kama ifuatavyo;

1.0. Dereva II - Nafasi 1

1.1. SIFA

- a) Elimu ya kidato cha nne (Form IV) yenye ufaulu wa somo la English na Kiswahili.
- b) Cheti cha mafunzo ya udereva kutoka chuo kinachotambulika (VETA, NIT au taasisi nyingine inayotambulika na Serikali).
- c) Leseni halali ya udereva ya Daraja C au zaidi kutoka Mamlaka ya Leseni za Udereva (TRA).
- d) Uzoefu wa kuendesha magari ya serikali au/na taasisi kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (3).
- e) Uelewa wa matengenezo madogo madogo ya gari (basic mechanical skills).
- f) Uadilifu, uaminifu, na uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu na mazingira yenye changamoto.
- g) Uwezo wa kufanya kazi kwa muda wowote, ikiwemo usiku, likizo au siku za mwisho wa wiki.

1.2. Kazi na majukumu

- a) Kuendesha magari ya hospitali kwa usalama na kufuata taratibu zote za usalama barabarani.
- b) Kuhakikisha gari lipo katika hali nzuri kila wakati na kufanya ukaguzi wa kila siku kabla ya safari.
- c) Kuwasafirisha wagonjwa, watumishi na mizigo ya hospitali kulingana na maagizo ya viongozi.
- d) Kuweka kumbukumbu za safari (log book) kwa usahihi.
- e) Kufanya matengenezo madogo madogo ya magari ya mara kwa mara na kwa wakati.
- f) Kuhakikisha na kusimamia matengenezo ya magari yaliyo kwenye utaratibu wa ratiba (regular services)
- g) Kuripoti mara moja changamoto zozote za kiufundi au ajali kwa uongozi.
- h) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

1.3. SIFA ZA UJUMLA

- a) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania: waombaji toka mikoa ya Lindi na Mtwara watapewa kipaumbele
- b) Wawe na umri wa miaka 25-35
- c) Waombaji wote watume maombi yao kwa njia ya maandishi yakiwa na:
 - Barua ya maombi ya kazi iliyoandikwa kwa mkono,
 - Nakala ya vyeti vya sekondari, elimu na mafunzo,
 - Nakala ya leseni halali ya udereva,
 - Nakala ya vyeti vya kuzaliwa na Kitambulisho cha Taifa (NIDA),
 - Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (Detailed CV) na picha ndogo za karibuni (passport size)
 - Waombaji wenye uzoefu waonyeshe taarifa za taasisi walizofanyia kazi pamoja na waajiri wao wasiopungua watatu (3)

NAMNA YA KUOMBA

Maombi yote yawasilishwe kwa;

MGANGA MFAWIDHI,
HOSPITALI YA RUFEE YA MT. WALBURGA NYANGAO,
S.L.P 1002,
NYANGAO, LINDI.

Maombi yanaweza wasilishwa kwa mkono kwa kuleta moja kwa moja au kupitia barua pepe nyangaohospital@gmail.com

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **23/11/2025**

